Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili - 00005809 Toleo 11: Septemba, 2013

Huduma bora za afya kwa watanzania wote

Utangulizi

KARIBU msomaji wetu katika toleo hili na 11 linaloelezea kwa ufupi baadhi ya shughuli za shirika zilizotekelezwa katika robo ya tatu ya mwaka huu (2013).

Sikika iliendelea kutekeleza shughuli za Ufuatiliaji na Uwajibikaji wa Jamii (Social Accountability Monitoring-SAM). Mara hii tulishiriki na kutoa uzoefu wa shirika kwenye kongamano la kimataifa la SAM ambalo liliwakutanisha wadau wapatao 150 kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizoko Kusini mwa Afrika (SADC). Wadau hao ni wale waliopata mafunzo ya uwajibikaji jamii. Washiriki walijadili mafanikio na changamoto zilizojitokeza kwenye utekelezaji wa SAM.

Naibu Waziri TAMISEMI, Mh. Aggrey Mwanri akizindua ripoti ya Utekelezaji wa SAM Tanzania. *(Picha kwa hisani ya Policy Forum)*

Shirika pia liliratibu mkutano wa wadau kutoka Tanzania Public Health Association-TPHA, Development Association for Tanzania (DATA) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa lengo la kujadili na kuweka pamoja mapendekezo ya Asasi za Kiraia (CSOs) kuhusu Afya katika rasimu ya Katiba Mpya. Kwa pamoja, walipendekeza Katiba Mpya ya Tanzania iweke kipengele maalum kinachotamka wazi kuwa **'Afya ni Haki ya Msingi ya kila Mwananchi'.**

Katika hatua nyingine, Sikika iliratibu mkutano wa timu ya SAM na watendaji wa Halmashauri ya Kibaha, mkoani Pwani na kutoa mrejesho wa shughuli ya SAM iliyofanyika mwishoni mwa robo ya pili ya mwaka. Vilevile, tulitembelea wilaya ya Iramba, mkoani Singida kuandaa filamu fupi ya mafanikio ya utekelezaji wa kazi ya SAM.

Kwa taarifa zaidi kuhusu kazi za Sikika, unaweza kupitia tovuti yetu; *www.sikika.or.tz, twitter- @sikika1, facebook- Sikika Tanzanianablogspot - www.sikika-tz.blogspot.com. Kwa maoni tafadhali wasiliana nasi kupitia info@sikika.or.tz au sms 0688-493-882.*

Ndani

Utekelezaji SAM – Wadau ndani na nje ya nchi waisifu Sikika..... 2
Haki ya Afya Izingatiwe Katiba Mpya 2
Wajipanga Kuboresha Huduma za Afya 3
Uongozi Iramba wapongeza kazi ya timu ya SAM 4

Haliuzwi

Utekelezaji SAM – Wadau ndani na nje ya nchi waisifu Sikika

Na Zakayo Mahindi

WADAU kutoka taasisi za The Guardian (Nigeria), Concern Universal (Msumbiji) na Zimbabwe Women Resource Center (Zimbabwe) wameipongeza asasi ya Sikika kwa mafanikio iliyopata ndani ya muda mfupi kupitia utekelezaji wa kazi ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii *(Social Accountability Monitoring*-SAM) katika ngazi ya jamii.

Wawakilishi wa taasisi hizo, Bw. Ajibola Amzat (Nigeria), Bw. Aly Elias Lala (Msumbiji) na Bi. Lindiwe Ngwenya (Zimbabwe) waliipongeza Sikika kwa kujenga uhusiano mzuri na serikali hasa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Iramba, hivyo kuleta mafanikio kwenye sekta ya Afya, ikiwemo upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na kadi za akina mama za kliniki bila malipo.

Mafanikio mengine ni utekelezaji makini wa miradi iliyopatiwa fedha, watoa huduma kuanza kutumia lugha nzuri kwa wagonjwa na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchangiaji Gharama za Afya inayotoa msamaha kwa wazee wenye miaka 60 na kuendelea.

Pongezi hizo zilitolewa Agosti mwaka huu (27- 29, 2013) kwenye kongamano la kimataifa la Uwajibikaji Jamii (Social Accountability Monitoring-SAM). Kongamano hilo liliwakutanisha wadau mbalimbali kutoka nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizoko Kusini mwa Afrika (SADC) na wengine waliopata mafunzo ya Uwajibikaji jamii, ili kujadiili mafanikio na changamoto zilizojitokeza kwenye utekelezaji wa mfumo huu.

Mshiriki mwingine katika mkutano huo, Bi. Edith Rukanga, kutoka Asasi ya EMEDO (Mwanza) aliipongeza Sikika kwa jitihada zake za kuboresha huduma za Afya nchini na kutaka kufahamu mbinu ilizotumia kupata mafanikio makubwa ndani ya muda mfupi.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Bw. Yahaya Nawanda ambaye aliwavutia wadau wengi kutokana na uelewa wake wa SAM na ushiriki makini alijibu; “Sikika walikuja kwenye wilaya yangu Iramba, wakajitambulisha, tukajadiliana juu ya utekekezaji wa SAM. Kwakuwa walinishirikisha na kwakuwa uwajibikaji ni moja ya kazi zangu za kila siku, nilisimamia zoezi mwenyewe,” alisema na kusisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa ukaribu na Serikali.

Bw. Nawanda pia alisifu utaratibu wa Sikika wa kutoa mafunzo kwa wananchi, kuwapa nyenzo za kufanya uchambuzi wa nyaraka na kisha kurudisha majibu kwa wadau. Alizitaka AZAKI nyingine kuiga mfano wa Sikika katika utekelezaji wa SAM.

Akifungua kongamano hilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mh. Aggrey Mwanri, alisema Serikali imevutiwa na kazi za kufuatilia na kusimamia rasilimali za umma zinazofanywa na AZAKI na kwamba Serikali inaunga mkono shughuli za kuwezesha wananchi kufuatilia na kudai uwajibikaji kutoka kwa viongozi na watoa huduma.

Naye Mh. Zitto Kabwe (MB) ambaye aliwasilisha mada ya utendaji wa Kamati za Bunge zinazosimamia Usimamizi wa Rasilimali za Umma, alitoa mfano wa kazi za Sikika juu ya Matumizi yasiyo ya Lazima na jinsi ambavyo uchambuzi wa taarifa zake unavyosaidia Kamati za Bunge katika utendaji. Aliziomba AZAKI kuongeza nguvu kwenye vita dhidi ya Uwajibikaji wa Serikali zao kwa umma.

Kongamano hilo liliratibiwa na mtandao wa AZAKI (Policy Forum) na lilikutanisha washiriki wapatao 150 kutoka nchi za Afrika ya Kusini, Zambia, Msumbiji, Zimbabwe, Nigeria, Kenya na Tanzania. Kongamano lilihudhuriwa pia na wajumbe kutoka Kamati ya Bunge ya SADC, Bunge la Tanzania, Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora ya Tanzania na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (CAG).

Haki ya Afya Izingatiwe Katiba Mpya

Na Mcharo Mrutu

ASASI za Kiraia zinazojishughulisha na utetezi wa masuala ya afya nchini zimependekeza Katiba Mpya ya Tanzania izingatie suala la afya ya binadamu kwa kuweka kipengele maalum kinachotamka wazi kuwa **‘Afya ni Haki ya Msingi ya kila Mwananchi’.**

Pendekezo hilo limetolewa Agosti mwaka huu, (2013) na wadau kutoka Tanzania Public Health Association-TPHA, Development Association for Tanzania (DATA), Sikika na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) wakati walipokutana kujadili na kuweka pamoja mapendekezo ya Asasi za Kiraia (CSOs) kuhusu Afya katika rasimu ya Katiba Mpya.

Akizungumza katika mkutano huo uliofanyika kwenye ofisi za LHRC, chini ya uratibu wa Sikika; Mratibu wa Katiba wa LHRC Bi. Anna Henga alisema pamoja na unyeti wa afya ya binadamu katika ustawi wa jamii yoyote ile, amesikitika kuona kwamba rasimu ya awali haikutilia maanani suala la afya.

“Haina maana kwa rasimu kuitambua haki ya kuishi bila kutambua haki ya kila mwananchi kupata huduma bora za afya,” alisema Bi. Henga na kutoa wito kwa wananchi na wadau kuipigania haki ya afya ili iingizwe kwenye

katiba mpya na kuacha kuwategemea wanasiasa na makundi mengine kwa kuwa yana vipaumbele tofauti.

Kwa pamoja, wadau hao walipendekeza kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuwa Haki ya Afya iwe Haki ya msingi katika Haki za binadamu inayopatikana katika sura ya nne ukurasa wa 16 na isomeke kama ifuatavyo:

1. Haki ya Afya (1) Kila mtu ana haki yakupata; (a) Elimu na taarifa sahihi juu ya masuala mbalimbali ya Afya, (b) Huduma zilizo bora za afya kwa gharama nafuu kulingana na mahitaji yake, (c) Fursa ya kupatiwa huduma ya kinga ya kiafya , (d) Fursa ya kushiriki katika tafiti za kisayansi/kiafya, (e) Huduma za dharura kama majanga na ajali.

(2) Ni **wajibu** wa kila mwananchi kutunza Afya yake, kushiriki na kusimamia masuala yanayohusu afya jamii. Pia serikali ya Jamhuri ya Muungano, mamlaka za nchi pamoja na taasisi zihakikishe uwepo wa vifaa tiba, vitendanishi na dawa kwa kila kituo kinachotoa huduma za afya na uwepo wa watumishi wenye weledi katika taaluma zao na kuzingatia maadili kwa kuzingatia ikama'.

(3) Kama ilivyo ndani ya katiba ya sasa ya Tanzania, rasimu ya katiba mpya nayo haikulipa uzito suala la 'Haki ya Afya' na badala yake limetajwa juujuu kwenye maeneo manne tu ambayo ni: Ibara ya 40, 42, 45 na ya 46 ambazo hazitoi nguvu za kisheria kuipigania haki hiyo mahakamani.

Wajipanga Kuboresha Huduma za Afya

Na Aisha Hamisi, Kibaha

UONGOZI wa halmashauri ya Kibaha, mkoani Pwani umepongeza kazi zinazofanywa na timu ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii (UUJ/SAM) kupitia uwezeshaji wa Sikika na kuahidi kuzipatia ufumbuzi hoja mbalimbali zilizoibuliwa wakati wa kazi ya ufuatiliaji wa upatikanaji wa huduma za afya, wilayani humo.

Miongoni mwa hoja zilizoibuliwa na timu ya (UUJ/SAM) baada ya kupitia nyaraka mbalimbali za mipango, ripoti za utekelezaji na kutembelea jumla ya vituo vya afya na zahanati 16 zilizopo Kibaha, ni pamoja na kuwepo kwa mapungufu kwenye mfuko wa afya ya jamii (CHF). Kwa mfano, timu hiyo ilibaini kuwa mchakato mrefu wa ununuzi wa dawa na vifaa tiba ndio chanzo cha uhaba katika vituo vingi vya huduma za afya. Ili kutatua hili, halmashauri imetoa mamlaka kwa vituo kupitia kamati za usimamizi, kutumia fedha za CHF kununua dawa na vifaa tiba kulingana na mahitaji.

Aidha, timu ya SAM ilibaini udhaifu katika mawasiliano baina ya halmashauri na wasimamizi wa vituo. Vituo havikupewa mrejesho wa taarifa za bajeti zililotolewa kwa vituo husika, hali inayoathiri ufanisi katika utoaji wa huduma.

UKIMWI ni suala mtambuka linalohitaji mikakati thabiti ya kupambana na kupunguza maambukizi katika jamii. Hatahivyo, timu ya (UUJ/SAM) Kibaha ilibaini muitikio mdogo wa halmashauri hususan katika kutumia fedha za ndani kutekeleza shughuli za UKIMWI. Kutokuingizwa bajeti za UKIMWI katika mipango ya afya, pia ni kikwazo katika kufikia malengo ya kitaifa juu ya janga hili.

Akizungumza kwenye mkutano wa majumuisho uliohudhuriwa na wadau mbalimbali akiwemo Katibu Tawala na Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kibaha Bi. Tatu Selemani alikiri kuwepo kwa changamoto hizo na kuahidi kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na timu ya (UUJ/SAM) katika mipango ijayo kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya wilayani humo.

Kwa kutambua umuhimu wa kazi ya (UUJ/SAM), Mwenyekiti wa Halmashauri Mh. Mansoor A. Kisebengo aliishauri Sikika kuangalia uwezekano wa kupanua wigo wa mafunzo na kuwezesha wananchi kufanya ufuatiliaji katika sekta nyingine za kijamii. *"Zoezi la SAM kweli linasaidia uwajibikaji na uboreshaji wa huduma, hivyo Sikika igeukie sekta nyingine ili kusaidia halmashauri kutoa huduma bora kwa wananchi"*

Awali, shughuli ya ufuatiliaji wilayani Kibaha ilianza Juni 03, 2013 hadi Juni 20 ambapo timu ya (UUJ/SAM)

ya wilaya yenye wajumbe 16 ilishiriki katika mchakato mzima. Timu hiyo ilihitimisha mchakato wa (UUJ/SAM) kwenye mkutano wa wadau. Lengo lilikuwa ni kutoa mrejesho kwa wadau wote na kuweka makubaliano juu ya namna ya kutatua changamoto zilizoibuliwa.

Uongozi Iramba wapongeza kazi ya timu ya SAM

Na Thomas Ludovick, Iramba

Uongozi wilayani Iramba, mkoani Singida umeunga mkono shughuli zinazofanywa na timu ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji wa Jamii (UUJ/SAM) katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya sekta ya afya, hivyo kuchangia uboreshaji wa huduma za afya.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya ya Iramba (DC), Bw.Yahya Nawanda wakati akizungumza na wadau wa sekta ya afya wilayani humo ambapo alisema kazi ya SAM imechochea jitihada zinazofanywa na serikali na wadau mbalimbali wilayani humo katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya.

"Hapo awali kulikuwepo mapungufu ya kiutendaji hasa kauli mbovu kutoka kwa baadhi ya wauguzi, lakini SAM imetufungua macho katika hilo," anasema DC Nawanda. Alieleza kuwa sulala hilo lilishughulikiwa haraka mara baada ya kuibuliwa wakati wa kazi ya ufuatiliaji wa timu ya UUJ/SAM na kwa sasa malalamiko kutoka kwa wagonjwa yamepungua.

Baadhi ya machapisho yanayopatikana Sikika

Aidha Bw. Nawanda alisema kuwa timu ya UUJ/SAM pia iliripoti juu ya tatizo la kutokuwepo kwa umeme katika vituo vingi vya kutolea huduma ambapo kwa sasa tatizo hilo nalo limepatiwa ufumbuzi. "Kwa sasa, asilimia mia moja ya vituo vya afya vimepata umeme, tofauti na awali".

Naye Dk. Jabir Juma ambaye ni Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Iramba, anakiri kwamba kabla ya UUJ/SAM, kulikuwepo na tatizo la uhaba pamoja na kuuzwa kwa kadi za klinikikwa wajawazito na watoto. "…tatizo hilo lilichangiwa zaidi na ucheleweshaji wa kadi hizo kutokana na mchakato wa kuziagiza kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) lakini mara baada ya UUJ/SAM tatizo hilo lilitafutiwa ufumbuzi na sasa kadi zinapatikana bure."

Aidha, Dk Juma alizungumzia changamoto ya uhaba wa watumishi katika vituo vingi vya kutolea huduma za afya kama ilivyoelezwa katika taarifa ya timu ya UUJ/SAM. "Suala la upungufu wa watumishi ni la kitaifa lakini tumejitahidi kupata watumishi wawili au zaidi kwa kila kituo,na tumefanikiwa kufanya hivyo."

Akizungumzia kazi ya SAM, mmoja wa wajumbe wa timu hiyo ambaye pia ni Diwani wa kata ya Mgongo, Bw. Kitundu Selemani alieleza kuwa UUJ/SAM imewajengea uwezo mkubwa wa kufuatilia kwa karibu masuala ya sekta ya afya katika maeneo yao na kuwahamasisha wananchi namna ya kuwajibika na kudai haki zao za msingi.

Sikika inaupongeza uongozi wa wilaya ya Iramba, kwa kutoa ushirikiano na kuzifanyia kazi changamoto mbalimbali katika sekta ya afya kwa lengo la kuleta mabadiliko na kuboresha huduma wilayani humo.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57

Ujumbe mfupi: 0688493882
Faksi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Faksi: 026 23 21316